# WATUMISHI HOUSING INVESTMENTS

6th Floor, Golden-Jubilee Tower
7 Ohio Street / Kibo Street
P.O. Box 5119
11481 Dar- Es Salaam -Tanzania

Tel : +255 22 2922211
Fax : +255 22 2922221
E-mail: info@whi.go.tz
Website: www.whi.go.tz

*Dar es Salaam, Tanzania.* *23/10/2024*

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

## Watumishi Housing Investments (WHI) yashinda Tuzo ya NYUMBA ZA GHARAMA MAFUU ZAIDI AFRIKA

Watumishi Housing Investments (WHI) imetunukiwa tuzo ya NYUMBA ZA GHARAMA NAFUU ZAIDI AFRIKA iliyotolewa na Taasisi ya Mikopo ya Nyumba Afrika (Africa Union for Housing Finance-AUHF) inayo tambuliwa na Umoja wa Afrika (Africa Union). Tuzo hiyo imetolewa katika Mkutano Mkuu wa AUHF mwaka 2024 uliofanyika Zanzibar hivi karibuni.

Tuzo hii ya heshima inatambua jukumu la WHI katika kuwezesha umiliki wa nyumba kwa watu wa kipato cha chini na kati nchini Tanzania na juhudi zilizofanywa na WHI katika kuleta suluhisho la njia nafuu za malipo za nyumba ikiwemo malipo endelevu yanayolipwa kipindi cha ujenzi bila riba pamoja na utaratibu wa mpangaji mnunuzi ambavyo vilitajwa kama sababu kuu za ushindi huu. Njia hizi zimeleta unafuu mkubwa sana kwa watu wanaotamani kumiliki nyumba. Nyumba za WHI zinauzwa kwa bei nafuu kwa kati ya asilimia 10 hadi 30% ikilinganishwa na nyumba kama hizo kwenye soko, huku bei ya kununua nyumba ikianzia shs milioni 38/=. Bei hizi pamoja na njia nafuu za malipo zimewasaidia Watanzania wengi kufikia ndoto zao za kumiliki nyumba.Tuzo hii pia inasherehekea kipindi maalum kwa WHI, kwani inatimiza miaka 10 ya ubunifu na uongozi katika sekta ya Makazi.

WHI inakuwa taasisi ya kwanza nchini na Afrika Mashariki kupokea Tuzo hii ya heshima. WHI iliibuka kinara kutoka kwa taasisi mbalimbali zinazohusiana na sekta ya makazi kutoka mataifa mbalimbali barani Afrika. Tuzo za AUHF zinatambua michango thabiti ya kuendeleza sekta ya makazi barani Afrika. Ushindi wa WHI ulitokana na utekelezaji wake wa kipekee katika kubuni na kutekeleza miradi ya nyumba yenye gharama nafuu zaidi na hivyo kuleta unafuu kwa wanunuzi ikiwalenga watumishi wa umma na wanachama wa mifuko ya hifadhi ya jamii.

Aidha, tathmini ilihusisha kuangalia kazi halisi iliyotekelezwa na WHI, pamoja na mazungumzo ya moja kwa moja na wanufaika wa miradi yake. Hii ilitoa fursa ya kupata maoni ya moja kwa moja kutoka kwa wananchi waliofaidika na miradi ya makazi ya WHI, ambapo walielezea jinsi njia nafuu za malipo zimewasaidia kufikia ndoto yao ya kumiliki nyumba.

AUHF, shirika muhimu linalounganisha wadau wa makazi barani Afrika kwa zaidi ya miaka 40, linawezesha washirika wake kuendeleza ufumbuzi zaidi wa makazi ya bei nafuu. Ahadi ya WHI ya kupunguza gharama za makazi na kutoa njia mbadala za malipo ilionekana kama hatua kubwa kuelekea kufikia maono haya.

Tuzo hii ni uthibitisho wa dhamira ya Serikali kupitia Ofisi ya Rais Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika kuwawezesha wananchi wake kupata makazi nafuu.

Watumishi Housing Investments ni taasisi ya umma chini ya Ofisi ya Rais UTUMISHI yenye jukumu la undelezaji wa milki na usimamizi wa mifuko ya uwekezaji wa pamoja. WHI inasimamia mifuko miwili yaani Mfuko wa Nyumba na Mfuko wa Faida Fund.

Imetolewa na;
**KITENGO CHA MAWASILIANO**